

## **UJUMBE WA SILO**

## **Maagizo kwa wachapishaji**

Ujumbe ulionenwa na Silo july 2002 ina sehemu tatu: Lile Kitabu, Lile Ujuzi, na Lile Njia.

Lile Kitabu kimejulikana kwa jina lingine la Sura ya Ndani.

Ujuzi imedhiririshwa kupitia kwa sherehe nane

Lile Njia ni msanyiko ya mawazo na fikira za watu.

Hili andiko ina ujumbe zote tatu. Unaweza kupata ujumbe hizi zikienezwa kwa njia ya vitabu na tepe au kanda.

© Silo. Second edition, 2007

**LILE KITABU**

## I. KUTAFAKARI

1. Hapa unaelezwa jinsi maisha yaliyopoteza maana yanaweza kugeuzwa yakawa yenye maana na ya kutoshelesha.
2. Hapa kuna furaha, upendo wa mwili, upendo wa vitu vya kugusika, upendo wa binadamu na upendo wa roho.
3. Hapa kafara, hisia kwamba una hatia na vitisho kutoka ngambo ya pili vinatupiliwa mbali.
4. Hapa maisha ya dunia hii hayapingani na maisha ya milele na milele.
5. Hapa unaelezwa kuhusu ufunuo wa kilindi. Ni katika ufunuo huu ambamo wote wanaotafakari kwa makini, wakitafuta kwa makini hufika.

## II. UTASHI WA KUELEWA

1. Najua unavyohisi kwa sababu naweza kufikiwa na hali yako. Lakini hujui kukabiliana na mambo ninayozungumzia. Kwa sababu hii, ikiwa nitakuzugumzia bila moyo wa kutaka utambue kile kinachomfanya mwanadamu awe na furaha na awe huru, unaweza kunufaika ukijaribu kuelewa.
2. Usifikiri kwamba utaelewa kwa kubishana nami. Unaweza kubishana ikiwa unaamini kwamba ukipinga ndipo utaelewa zaidi, lakini njia hiyo haifai katika swala hili.
3. Ukiniuliza hali inayofaa, nitakwambia kwamba ni kutafakari sana na bila haraka kuhusu yale yaliyoelezwa hapa.
4. Ukijibu kwamba unakazi ya kufanya haraka zaidi, nitajibu kwamba sifanyi chochote kukupinga kwa maana ni matilaba yako kulala au kufariki.
5. Wala usiseme kwamba hupendi mtindo wangu wa kueleza mambo, kwani huwezi kulilaumu gand hali unalipenda tunda.
6. Nasema mambo kwa njia ninayoidhania bora, sio vile wanavyotaka wale wanaotamani vitu vilvyo mbali na ukweli wa ndani.

### III. KUPOTEA KWA MAANA

*Baada ya siku nyingi niligundua hiki kitendawili kikubwa: wale walikuwa na hofu wa kuanguka, walishinda hatimaye, ili wale walijivunia wameshinda waliachwa kando ya njia kama mimea ambayo maisha yake imetolewa na kutupwa. Baada ya siku ayami, nikiibukia kutoka ndani la giza kuu, niliifikia nuru, nikiongozwa na tafakari na wala si kwa mafunzo.*

*Hivyo nikajiambia siku ya kwanza:*

1. Hamna maana katika maisha ikiwa kila kitu kitakoma kwa kifo.
2. Kudhibitishwa kwa matendo kuwa ya haki, hayo matendo yawe ya kuaibisha au yawe ya kupendeza, siku zote ni ndoto mpya ambayo huacha utupu peke yake mbele.
3. Mungu amedhibitishwa kuwepo.
4. Imani ni kitu kinachobadilika kama akili na ndoto.
5. “Kile mtu anachopaswa kufanya” ni swala ambalo linaweza kujadiliwa kwa mapana na marefu, lakini hatimaye hakuna kitu kinachounga mkono hoja lolote.
6. “Jukumu” la wale wanaoahidi kutekeleza wajibu fulani si kubwa kuliko jukumu la wale wasioahidi.
7. Natenda kulingana na matakwa na mahitaji yangu, na hili halinifanyi mwoga wala shujaa.
8. “Vitu ambayo yananipendeza” hayadhibitishi ukweli wala kudharauliwa kwa mambo yote.
9. “Sababu zangu” si afadhali kuliko sababu za wengine, na sio hafifu zaidi.
10. Ukatili hunitia hofu, lakini si kwamba ukatili ni bora zaidi au hafifu zaidi ya wema.
11. Kile ninachosema au wengine wanachosema leo hakina thamani kesho.
12. Kufariki sio bora kuliko kuishi wala kutozaliwa kamwe, na sio mbaya zaidi.
13. Niligundua, sio kwa mafunzo bali kwa kuona na kuwaza, ya kwamba hakuna maana ya kuishi ikiwa kila kitu inaishia kwa kifo.

#### IV. KUJITEGEMEA

*Siku ya pili.*

1. Hakuna chochote ninachokifanya, kuhisi au kuwaza kinachonitegemea mimi.
2. Naweza kubadilika na nina tegemea vitendo vya mazingira yangu. Nikitaka kubadilisha mazingira yangu au “nafsi yangu” ni mazingira yangu yanayoishia kunibadilisha. Halafu natafuta mji mpya au vitu vya kugusika, ukombozi wa watu wote au kupigana upya kudhibitisha kuishi kwangu. Kwa namna yoyote ni mazingira yangu yanayo niongoza kuchagua mwelekeo mmoja au mwingine. Kwa njia hii, matumainio yangu na mazingira yangu huniacha hapa.
3. Nasema, kwa hivyo, si hoja ni nani ama nini itakayoamua. Katika matukio haya nasema kwamba sharti niishi kwasababu niko katika hali ya kuishi. Nasema haya yote, lakini hakuna chochote kinachodhibitisha ukweli au uhakika wake. Naweza kukata shauri, kusitasita, ama kubakia nilipo. Kwa namna yoyote, kitu kimoja ni bora kuliko kingine kwa sababu ni cha sharti, baadaye hakuna kilicho bora au baya zaidi.
4. Mtu akiniambia kwamba wasiokula hufa, nitajibu kwamba ni hakika, na kwamba, wakichochea na mahitaji yao, wanalazimika kula. Lakini sitaongeza kwamba kung’ang’ania kula hudhibitisha umuhimu wa kuishi kwa mtu – na sitasema kwamba ng’ang’ano hili ni baya. Kwa urahisi nitasema kwamba lote hili humhusu mtu binafsi ama ukweli wa kutaka kuishi, lakini hilo halina maana wakati unaposhindwa kwa vita la mwisho.
5. Nitasema, kwamba nina uhusiano na watu masikini, wanaogandamizwa na wanaodhulumiwa. Nitasema najisikia “utoshelevu” katika uhusiano huu, lakini naelewa ya kwamba hisia hizi hazidhibitishi chochote.

## V. KUTAMBULISHWA KWA MAANA

*Siku ya tatu.*

1. Wakati mwingine nimetazamia kimbele mambo yaliotukia baadaye.
2. Wakati mwingine nimelielewa wazo lililo mbali.
3. Wakatu mwingine nimezieleza mahala ambazo sijawahi kuzizuru.
4. Wakati mwingine nimeeleza bila kukosea yale yalivyotukia wakati nikiwa sipo.
5. Wakati mwingine furaha ghaya imenishangaza.
6. Wakati mwingine ufahamu kamilifu wa kila kitu umenijaza furaha.
7. Wakati mwingine kunena kikamilifu na kila kiumbe kimenijaza furaha.
8. Wakati mwingine nimeshinda nguvu ndoto zangu na kuuona uhalisi katika njia mpya.
9. Wakati mwingine nimeona kitu kwa mara ya kwanza lakini nikakitambua kana kwamba nilikuwa nimekiona awali.

*Na haya yote yamenifanya nifikirie. Ni wazi kwangu kwamba bila takriba hizi, singeibuka kutoka kwenye kupotea kwa maana au umuhimu.*



## VI. KULALA NA KUAMKA

*Siku ya nne.*

1. Siwezi kuchukulia kuwa halisi kile ninachokiona katika ndoto zangu, au kile ninachokiona nikiwa nimechukuliwa na usingizi mwepesi, ama kile ninachokiona nikiwa silali lakini niko kwenye mawazo mazito.
2. Naweza kuchukulia kuwa halisi kile ninachokiona nikiwa macho na bila mawazo mazito. Hapa sizumgumzii juu ya kile hisia yangu hunakili, kwa sababu ujumbe wenye uzuzu na wa upotevu unaweza kuletwa na hisia za nje na zandani, na pia kutoka kwenye mambo yaliopita. Hasa nazumgumzia shughuli za akili zangu kwa jinsi zinavyohusiana na ujumbe unaoletwa. Kile kilicho dhabitit ni kwamba wakati akili yangu hailali “inajua” na wakati imelala “inaamini”.kwa wakati mwingine nina fahamu ukweli kwa njia mpya, na ni wakati huo nina tambua ya kwamba, kile hua nikiona inafanana na usingizi au usingizi-mwepesi.

*Kuna njia halisi ya kukaa bila kulala, na imeniongoza kutafakari kwa uzito kwa yale yote tumenena mpaka sasa.kwa maana nyingine imenifungulia mlango wa maana ya vitu vyote vilyomo.*

## VII. UWEPO WA LILE NGUVU

*Siku ya tano.*

1. Nilipokuwa macho kweli nilikwea kutoka ufahamu mmoja hadi mwingine.
2. Nilipokuwa macho kabisa lakini nikakosa nguvu ya kupanda, niliweza kuuteka ule nguvu kutoka ndani yangu. Nguvu huu ulikuwepo katika mwili wangu wote. Nguvu yake yote ilikuwa kwa chembechembe ndogo wa mwili wangu, na ilizunguka kwa kazi na ushindo zaidi ya damu yangu.
3. Niligundua ya kwamba lile nguvu lilijisanya mahala fulani katika mwili wangu wakati sehemu zile zilikuwa na nguvu, na zilikosa nguvu wakati nguvu ilikosekana.
4. Nikiugua lile nguvu lilikosekana au lilijisanya hasa kwenye sehemu za mwili wangu zilizodhurika. Lakini ikiwa ningeweza kuanzisha utirikaji wa kawaida wa lile nguvu, magonjwa mengi yalianza kutoweka.

*Watu wengi walifahamu haya, na kupitia taratibu mbalimbali ambazo zinaonekana kuwa za ajabu kwetu leo, waliweza kuanzisha tena utirikaji wa lile nguvu.*

*Watu wengi walijua haya, na waliweza kupeana nguvu hii kwa wengine, wakileta "mianga" ya ufahamu na pia "miujiza" inayoonekana kwa macho.*

## VIII. KUIWEKA LILE NGUVU CHINI YA MAMLAKA

*Siku ya sita.*

1. Kuna njia ya kuiongoza na kulifanya lile nguvu lisanyike mahali pamoja wakati lile nguvu lina zunguka mwili yote.
2. Mwilini kuna sehemu za mamlaka ambayo inafanya mwili isonge, iwe na miasho na iwe na. Nyakati lile nguvu linasanyika katika mahali hizi, inafanya mwili iwe na joto, miasho na akili ya kuonekana.
3. Ikitegemea na vile lile nguvu linatenda kazi ndani au nje zaidi katika mwili, hali za usingizi wa pono, kusinzia au kuwa macho huibuka. Kwa hakika, zile duara za nuru zinazoizunguka miili au vichwa vya watakatifu (ama wale watukufu waliozindukana) katika michoro ya kidini huashiria tukio hili la nguvu lile ambayo wakati mwingine hujionyesha nje hadharani.
4. kuna sehemu ya mamlaka ya kuwa macho-kwa-hakika, na kuna njia ya kuleta lile nguvu mahala hapa.
5. Lile nguvu likiletwa mahala hapa, mahali zote za mamlaka zinasonga kwa njia mpya.

*Baada ya kuelewa hii na kutupa lile nguvu kwenye ncha hii bora, mwili wangu mzima ulihisi kishindo cha nguvu kubwa. Hili nguvu lilianguka kwa kishindo ndani ya ufahamu wangu, na nikapanda kutoka uelewaji mmoja hadi mwingine. Lakini pia niliona kwamba ikiwa ningepoteza udhibiti wa lile nguvu ningeteremkia vina vya akili. Halafu nilikumbuka hadithi za "peponi" na "jehanamu" na nikaona mstari unaogawanya hali hizi mbili.*

## IX. UDHIRISHAJI WA LILE NGUVU

*Siku ya saba.*

1. Nguvu hii iliyo katika mwendo ingeacha kuutegemea mwili na bado idumishe umoja wake.
2. Msanyiko wa hili nguvu kwa kweli ilikuwa kama “umaradufu” wa mwili ikilinganishwa na picha ambayo inawakilisha mwili wa mtu binafsi ndani ya nafasi ya kuwakilisha. Sayansi zinazoshughulika na mambo ya kiakili havijawapa mawazo ya kutosha kwa uwepo wa hili nafasi au uwakilishaji unaolinganishwa na miasho ya kilindi wa mwili.
3. Nguvu ambayo imeongezeka maradufu kama hii-ambayo inafikiriwa ni kama iko “nje” wa mwili au “umetenganishwa” kutoka kwa umbo lake-aidha imeyeyushwa kama mfano au kuwakilishwa vizuri, ikilingana na muungano wa kilindi wa yule anatekeleza kazi hili.
4. Niliweza kuyakinisha kwamba “uwekaji wa nje” wa hili nguvu – ambao uliwakilisha mwili wa mtu kama yuko nje ya mwili wake – unaweza kutekelezwa hata kutoka kwenye viwango vya chini kabisa, vya akili. Katika kadhia hizi, tisho kwa muungano wa ki msingi kabisa wa viumbe vilivyo hai lilileta itiko hii ili kumkinga yule aliyekuwa hatarini. Ndio sababu, katika maono wa baadhi ya vijumbe ambavyo viwango vyake vya ufahamu viko chini na umoja wake wa ndani umeponzwa, itikio hizi zilitokea bila ya kupangiwa na haikujulikana kwamba zimejileta zenyewe, lakini zilidhaniwa kuletwa na vitu vingine.

*“Vizuka” vya watu Fulani, kama “roho” za baadhi ya watabiri, zilikuwa si chochote si lolote lakini ni “rudufu” (kujihainisha) kwa wale waliojihisi kuwa na pepo. Baada ya kupoteza udhibiti wa lile nguvu, hali yao ya akili ilitiwa kisa katika usingiza mzito, na walijihisi kutawaliwa na viumbe vya ajabu ambavyo wakati mwingine vilileta matukio ya ajabu. Bila shaka hii ilikuwa ndiyo hali ya wengi waliotajwa kuwa na pepo. Kilichokuwa dhahiri, kwa hivyo, ni udhibiti wa lile nguvu.*

*Lote hili lilibadilisha kabisa mawazo yangu kuhusu maisha ya kila siku na maisha baada ya kifo. Kupitia kwa mawazo haya na tafriba hizi nilianza kupoteza imani katika kifo, na sasa sina imani yeyote katika mauti, vile tu ambavyo sisadiki tena ukosefu wa maana na ya maisha.*

## **X. KUDHIBITI MAANA**

*Siku ya nane.*

1. Umuhimu halisi wa maisha yaliyozindukana ulijidhirisha kwangu.
2. Umuhimu wa kuondosha farakano ya kilindi yalikuwa dhahiri kwangu.
3. Umuhimu halisi wa kuelewa lile nguvu ili kupata ushirikiano na mwendeleo ulinijaza furaha lenye maana.

## XI. KATIKATI ING'AAYO

*Siku ya tisa.*

1. Ndani ya lile nguvu Katika mlikuwa na “lile nuru” iliyotoka kwenye “katikati fulani”.
2. Mradi tu unatoka kwenye lile katikati, lile nguvu lina rudi chini, lakini ukiweka pamoja lile nguvu na kuunganisha lile nguvu, lile katikati i'ngaayo linatenda kazi.

*Sikuona ajabu kukuta watu tofauti wa zamani wakiabudu jua. Na niliona kwamba wakati baadhi ya watu waliabudu kitu hiki cha juu kwa sababu kilizipa dunia na asili maisha, wengine waliitambua kitu hicho cha kuheshimiwa mfano wa kitu kinacho dhaminiwa.*

*Kuna wale walioenda mbali zaidi na kupokea zawadi zisizohesabika kutoka kwenye katikati hii, tuzo ambazo wakati mwingine “ziliteremka” kama ndimi za moto katika wale waliofunguliwa heri, wakati mwingine ilifika kama duara inayong'aa, na wakati mwingine ilitokea kama misitu inayochomeka mbele ya yule muumini mwenye hofu.*

## XII. YALE MAVUMBUZI

*Siku ya kumi.*

*Mavumbizi yangu yalikuwa machache lakini muhimu, na ninayasema kwa maneno machache hivi:*

1. Ingawa msukumo ule huenea mwilini wenyewe, unaweza kusimamiwa kupitia kwa juhudi inayohisiwa. Kufanikiwa kupata badiliko lililokuhusudiwa katika kiwango cha ufahamu humpa mwanadamu tazamo muhimu la uhuru kutoka kwa zile hali za “asili” ambazo huonekana kujipasha katika ule ufahamu.
2. Katika mwili kuna sehemu ambazo hudhibiti utendaji wake tofauti.
3. Kuna tofauti baina ya hali ya kuwa macho na hali ya viwango vingine vya ufahamu.
4. Msukumo ule unaweza kuongozwa kufikia kiwango cha kuamka wa kweli (kuelewa kwa “msukumo” nguvu ile ya kiakili ambayo huandamana na mchoro mahsus na kwa “ncha” ulipo mchoro wa aina hiyo katika “mahali” fulani kwenye nafasi ya uwakilishaji).

*Kutanabahi huku kote kuliniongoza kutambua katika dua za watu wa zamani mbegu ya kweli adhimu – kweli ambayo baadaye ilifumbwa na matendo ya ibada na desturi za nje, ikizifanya zisiweze kukuza ile kazi ya ndani ambayo, ikitambulika kwa ukamilifu, huwaweka watu kushikamana na usuli wao ung’ao.*

*Mwishowe, nilitanabahi kwamba “mavumbuzi” yangu hayakuwa mavumbuzi kwa vyovyote, lakini yaliinuka kutoka kwenye ule ufunuo wa ndani ambao kwao hufika wale ambao, bila ukinzani, hutafuta ile nuru katika mioyo yao wenyewe.*

### XIII. MASHARTI

*Maisha na vitendo huwa tofauti wakati utu wa ndani unafunuliwa kama radi.*

*Ukifuata maagizo pole pole`ukitafakari juu ya yale yamenenwa na yale yajao, unaweza kubadilisha yasiyo na maana yakawa na maana.*

*Yale unafanya na maisha yako sio ya kigeni. Maisha yako ambayo iko chini ya sheria ina mambo mengi ambayo unaweza kuchagua.*

*Si waongeleshi juu ya kukombolewa bali juu ya ukombozi, maandamano na hatua kwa hatua. Si waongeleshi juu ya kukombolewa kama kitu kikamilifu bali juu ya kujikomboa hatua kwa hatua, kama wasafiri ambao wameona mji walio tarajia kufika wanaokolewa kwa njia ndefu walikotoka. Kwa hivyo kile-ambacho-mtu-lazima-afanye haitegemei urefu wa safari, ugumu wa kuelewa na tabia ya kawaida, lakini kwa sheria: sheria ya uzima, nuru na kuelewa kwa utaratibu.*

*Hapa kuna yale masharti tayari tuli taja yanayo weza kukusaidia kutafuta ushirikiano wa kilindi.*

1. Kuenda kinyume cha utaratibu wa vitu vya ulumwengu ni kuenda kinyume chakobinasfi.
2. Ukilazimisha kitu ikamilike kabla ya saa yake, uta vuna usichojitarajia.
3. Usiende kinyume cha nguvu nzito. Ngoja nguvu yake irudi chini, halafu uishinde kwa akili timamu.
4. Mambo yako sawa vitu vikitendeka pamoja, sio kwa upwekwe.
5. Ikiwa mchana na usiku, wa kati wa jua au wakati wa baridi ni sawa kwako, basi umeshinda kupigana kwa mawazo.
6. Ikiwa unakimbilia maisha mwororo, unajiumiza mwenyewe. Lakini ikiwa hufanyi Madhara yeyote kwa maisha yako, ponda raha wakati unaweza.
7. Ikiwa una kimbilia mwisho wa vitu, unajifunga mwenyewe. Ikiwa kila kitu unafanya unaona ni kama umekamilisha kazi yako, una jikomboa.
8. Utafanya furukano zako zipotee ikiwa utayaelewa penye zilianzia, sio ukitaka kuya tatua.
9. Ikiwa unaumiza wenzako, unajifunga mwenyewe, lakini ikiwa huumizi mtu yeyote, unaweza kutenda vile unapenda.
10. Ikiwa unatendea jirani yako vile ungependa wa kutendee, unajikomboa mwenyewe.



11. Haijalishi ni wapi dunia imekuweka, kilicho muhimu ni kujua ya kwamba, haukuchagua kwenye ulipo.

12. Farakano ama umoja yamo ndani yako. Ukirudia mambo yako ya umoja ilioko ndani yako hakuna kitu itakufunga.

*Utakuwa kama nguvu ya maumbile ambayo haijapata kizuizi mbele yake. Tambua tofauti kati ya mambo magumu , matatizo, kizuizi na furugano. Ingawa hayo mambo mengine yatakufanya uendelee mbele au kuwa na miasho, furugano inakufunga kwa mviringo bila njia ya kujiokoa.*

*Saa yeyote ukipata nguvu zaidi, furaha na upendo moyoni mwako, ama ukijisikia huru bila furugano, ushukuru kwa kilindi bila kuchelewa. Ukijikuta katika mambo ambayo yana tofautiana, uliza kwa imani, na yale mazuri yote uliyopanda yatakurudia yakiwa yame badilishwa na kuongezeka kwa mafanikio.*

#### XIV. KUONGOZWA KWA NJIA YA NDANI

*Ikiwa umeelewa yale nime kueleza mpaka sasa, basi unaweza kuhisi matendo ya hili nguvu ukifanya hili zoezi ndogo. Sio sawa na kutafuta ukweli wa akili timamu (ni kama hili ni swali la kutafuta njia ya kufanya kazi ya kiteknologia) ni kama kuingilia miasho fulani na kuongea wasi wasi inayoletwa na shairi. Lugha inayotumika kueneza hizi ukweli, inatumika kueneza mienendo inayefanya mtu awe katika uwepo wa mawazo ya kilindi badala ya kuwa katika uwepo wa miasho ya “uwepo wa mawazo”.*

*Sasa fuata kwa makini yale nitakacho kuelezea, kwa sababu inahusu pahali wazi ya kilindi ambaye unakutana naye wakati unafanya na lile nguvu na njia unayechora kwa mienendo cha akili chako.*

*“Katika njia ya kilindi unaweza kutembea kwa giza au kwa mwangaza. Fuata barabara zote mbili ambazo yatafunguliwa mbele yako.*

*Ukujiwacha utembe katika giza, mwili wako inashinda vita na inatawala. Halafu utakuwa Na mambo mengine yatatokea Kama: kuonekana kwa mapepo, nguvu, na mawazo ya mambo yaliopita yatatokea. Katika hili barabara enda chini kwa chini. Hapa panaishi chuki, kulipa kiasi, vitu ambavyo huyafahamu, uridhi, sugu na uta tamani kubaki papo hapo. Ukuzidi kuenda chini zaidi, utavamiwa na kuudhika, utajichukia na ndoto na matumaini yote ambayo imeleta uharibifu na kifo kwa binadamu yatakuvamia.*

*Ukijielekeza katika mwangaza, utapata mazuizi na uchovu katika kila hatua. Kuna vitu utalaumu kwa uchovu ukiendelea kupanda. Maisha yako, mawazo ya mambo yaliopita, kupanda inazidi kuwa ngumu na matendo ya mwili wako ambayo inaonekana ni kama ndio ianongoza.*

*Katika hatua ya kupanda utapata mahali hujawai kouna na rangi tofauti na milio ya sauti hujawai kusikia.*

*Usi kimbie utoroke kujitakaza, ambaye inafanana na moto na ina kushutua kama nyati (kitu cha kuogofia).*

*Usikubali kushutuliwa na usife moyo.*

*Usikubali tamaa ya kukimbia kwenda kwa mteremko na kwenye giza.*

*Usikubali kuyakumbuka mambo yaliopita.*

*mamilioni-ya –rangi inatiririka katikati ya wimbo yasiojulikana zikielekea mji wa meza na maua.*

*Usiogope Mwangaza takatifu yanapambazuka juu ya mlima wa minyororo, na maji-yenye-lile mwangaza ambayo inakusukuma nyuma ikiongeza uzito wake wakati unaingia katikati yake. Inyue sawa sawa ni maji au mawimbi—kwa sababu, ndani yake kuna uzima.*

*Ukipata hili mji uliofichwa ndani ya mlima wa minyororo, lazima ujue mlango wake—na utaijua wakati maisha yako yatabadilishwa. Ukuta zake ambazo ni kubwa*

*zimeandikwa kwa herufi, ambayo pia zimeandikwa na rangi, yana "hisiwa". Ndani ya mji huu pamewekwa yale yametendwa na yale-yata-tendwa. Lakini kwa macho yako ya kilindi, yalioonekana hayaonekani. Ndio, ukuta hayapitiki kwako!*

*Chukua nguvu ya huo mji uliofichwa. Rudi katika ulimwengu uliofifia ikiwa uso na mkono wako yana'ngara."*

## XV. KUHISI AMANI NA NJIA YA NGUVU

1. Nyoosha mwili wako na utulize fikira zako. Halafu, fikiria, wingu ambaye unaweza kuona ndani yake ikikujia kwa njia ya utaratibu mpaka ifike na ijipumzishe katika roho yako. Kwa hiyo saa utafahamu ya kwamba lilo wingu linakoma kuwa kama kitu na inajigeuza kuwa miasho katika kifua chako.
2. Angalia vile miasho ya lile wingu linapanuka pole pole kutoka kwa moyo wako ikienea nje wa mwili wako, wakati kupumua kwako kinazidi kuwa mazito na ya kindani. Wakati miasho yanafika ukingoni wa mwili wako, unaweza kukoma hapo na usikie amani wa kilindi. Unaweza kukaa hapo kwa mda vile inakupendeza. Kukamilisha, ukiwa mnyenyekevu na mwenye nguvu, rudisha lile nguvu pole pole, mpaka ifike kwa roho yako vile ulianza hadi lile wingu litoke nje vile lili ingia pale mwanzo. Hili tendo linaitwa kuhisi amani.
3. Ikiwa unataka kuhisi njia ya lile Nguvu, lazima uzidi kuipanua badala ya kuirudisha chini, ukiruhusu mawazo yako na mwili wako wote iende pamoja nawe. Usijaribu kuweka mawazo yako kwa kupumua kwako; iache ienee peke yake wakati unafuata kupanuka kwa lile nguvu nje wa mwili wako.
4. Wacha ni rudie: mawazo yako yote kila wakati lazima iegemee katika lile wingu ambayo lina zidi kupanuka. Ikiwa huwezi kukamilisha tendo hili, ni heri ukome na ujaribu tena siku nyingine. Ikiwa hautafaulu kupata lile njia ya nguvu utafaulu kupata lile miasho matamu ya amani.
5. Ikiwa utaendelea zaidi, uta weza kuhisi njia ya nguvu. Miasho kutoka kwa mkono wako na mahali pengine pa mwili wako yatakuwa yanajisikia tofauti. Baadaye unaweza kusikia miasho ikiongezeka, na mda si mda utaona vitu na upendo mwingi unaweza kutokea. Acha hili njia lienee...
6. Ukipata hili nguvu, ikitegemea na tabia yako ya ndoto, utaona nuru au sauti mbali mbali. Kilicho muhimu ni kuhisi uwepo mkubwa wa mazingira zako ya kiroho, ambayo yana onyeshwa na uwepo wa kuilewa kile kinaendelea.
7. Ikiwa hali hii haitaisha mda unapozidi kuenea, unaweza kuifanya imalizike saa yeyote unafikiria au kusikia lile wingu liki songa songa na kukuacha vile lilingia hapo awali.
8. Ni ya muhimu kujua ya kwamba, mabadiliko mengi ya mazingira ya kiroho yamekuwa yakipatikana kutokana na matumizi ya matendo ambayo tuliyataja hapo awali. Haya yana weza kufichwa na matendo yasiyo ya kawaida, au yana weza kuongezwa nguvu na mambo kama kusikia uchovu mwingi, kurudia rudia matendo fulani na kusimama kwa njia inayo badilisha kupumua na kuharibu miasho wa mwili.

Kwa hii uwepo inafaa utambue, mambo ya kufanya mtu awaze yaliopita, watu ambao wana wasiliana na wafu, na maradhi yanao letwa na dawa ya kulevia—yote ambayo ingawa yana tumia njia tofauti yana tupa majibu sawa. Ukiona haya yakitendeka, ina maanisha kwamba, hauna uwezo wa kujikinga na hujui yanachotendeka. Usi amini haya matendo, walakin yazione tu kama maono yenye watu wengine kama, wajinga na (tukisoma ya kale) “watakatifu” wame ya pitia.

9. Hata Kama umefuata maagizo haya, kuna uwezo ya kwamba hukufaulu kupata njia ya Nguvu hili. Hili lisiwe kama vikwazo bali uichukue tu kama kidhiririsho ya kwamba hujaiachilia mafikira zako za ndani itawale, ambayo ni dhiririsho ya kupigana kwa ubongo au matatizo na yale maono—kwa kumalisha, utafarakana na matendo ya kindani—kitu ambacho, haitaisha hapo, lakini itakuwa kwa maisha yako.

## XVI. KUDHIRIRSHA KWA LILE NGUVU

1. Ikiwa umehisi Njia Ya Nguvu, uta tambua ya kwamba, kulingana na kuhisi mambo mengine kama hili uliyoyapitia bila kujua, watu wengi wameanzisha, urogi na dini ambayo badaye yameenea zaidi. Kulingana na kuhisi mambo kama haya ambayo tumetaja hapo hawali kuna wengine walijisikia ya kwamba mwili wao ulikuwa ulijiongeza “ukubwa mara mbili” na kuhisi kwa lile Nguvu liliwapa miasho ya kudhania wangeweza kuelekeza hili nguvu nje wa mwili wao.
2. Lile Nguvu “lingeelekezwa” kwa wengine na pia kwa maumbo ambayo “yametengenezwa” kuikaribisha na kuiweka isiharibike. Nina amini haitakuwa ngumu kwako kuelewa matendo ya madhehebu mbalimbali, na maana ya pahala patakatifu na wahubiri “waliojazwa” na Nguvu. Wakati maumbo fulani walizingirwa na sherehe na utaratibu na kuomba kwa imani katika makanisa, hakika “walipeana” kwa waamini lile nguvu lilisanywa kutokana na maombi ya sio koma. Kwa vile kuhisi ya kilindi kinatakikana kukielewa hili jambo, kujaribu kuelewa, ambayo yanategemea mambo ya nje, yanafunua vile hatuna ufahamu wa ukweli wa binadamu—ingawa haya mambo ya nje ni utamaduni, giografia, historia au mambo ya kale.
3. “Kuelekeza”, “kuipatia nguvu”, na “kuiiongeza” hili Nguvu ni mambo ambayo tuta ya rudia baadaye. Kwa hivi sasa, wacha niseme ya kwamba haya mambo yanazidi kuenea katika mazingira ya viongozi na wengine ambao wana vutia watu kwa njia moja au nyingine wakiwa wame vutia watu ambao wana tamani tu kuwagusa, kupata kijipande cha nguo chao, sehumu kidogo cha mali yao ama tu kuwaona.
4. Hili linatendeka kwasababu mawakilisho yote ya “urefu” yanapanuka kutoka kwa sehemu la jicho likiendelea juu, likipita hali ya kawaida ya kuona vitu. Na waliyo ona “juu zaidi” ni wale “walio pata” ukarimu, uwerevu na nguvu. Pale ndani, “juu” pia tuna pata utaratibu wa waongozi, nguvu yalioko na bendera ya mataifa. Na sisi wengine ni lazima, kwa kila njia, tupande ngazi ya umarufu ili kufike karibu na lile nguvu. Tunajikuta katika hali mbaya, bado tukiwa chini ya utawala ya haya mambo ambayo yanalingana na kujiwakilisha kwa ndani, vichwa vietu vikiwa mle “juu” na miguu zikikwama chini. Tunajikuta katika hali ya kujihuzunisha ikiwa tutayaamini mambo haya na kuya-amini kwasababu zina msingi ya kujiwakilisha kwa kindani. Tunajikuta katika hali ya kusikitisha, ikiwa sura yetu ya nje inatofautiana na lile sura ya ndani.

## **XVII. KUPOTEZA NA KURUDI CHINI KWA LILE NGUVU**

1. Kutoweka kwa hili nguvu linalingana na matendo yasio pimwa, yakiwa; mawazo, upelelezi isiopimwa, kuongea bila kipimo, mapenzi bila kipimo, kudhania—kuangalia, kusikiliza, kuonja na kadhalika, kwa matendo yasio na maana. Lakini inafaa utambue ya kwamba watu wengi hutenda hivi kwa maana ina wafanya watoe mawazo ambayo yana dhuru maisha yao. Tukiangalia mambo yote na tukiona matendo ya kutoweka kwa lile nguvu, nina hakika utakubaliana nami ya kwamba haina maana kuzirudisha chini bali kuziamuru zitulie.
2. Tukiongea kuhusu mapenzi, lazima utafsiri vizuri: hili jambo halifai lirudishwe chini, Kwasababu italetu uchungu na farakano wa kilindi. Mapenzi inajielekeza kwa na kumalizika kwa kitendo na haina faida ikizidi kuwa kwa mawazo au ikiendelea bila kukoma kikitafuta kiumbe cha kupenda. Kuweka mapenzi chini ya sheria na watu fulani au utakatifu wa dini yamefanya mapenzi kutofautiana na maumbile.
4. Kwa mataifa ambayo hili nguvu limerudishwa chini (lile nguvu ya kuwakilisha miasho ya mwili) limerudishwa nyuma likiangalia giza. Katika hayo mataifa, mambo mengi yameongezeka kama, “kushikwa na mapepo”, “wachawi”, wanaojifanya na ukorofi wa aina mingi ambao wanasherehekea kuona watu waki taabika na uharibifu wa maisha na urembo wa dunia. Katika makabila na miji mengine wakorofi walipatikana kati ya wale wanahatia na wale hawana hatia. Kwa mambo mengine, yote ya kisayansi na maendeleo ilisulubiwa kwasababu ilipinga kutokuwa na usawa, lile giza na waliozuiliwa.
5. Kufinyilia kwa mapenzi bado yako katikati ya watu wasio “chanuka”, vile tu inafinyiliwa kati ya wale tunadhania “wamechanuka” ina onekana dhahiri ya kwamba ingawa yote mawili yana mwanzilishi tofauti, yote yana kabiliwa na madhara makubwa.
6. Ukiniuliza nieleze zaidi, nitakwambia ya kwamba, kwa kusema kweli, mapenzi ni takatifu na ndio mwanzo penye uhai na viumbe vilitokea, vile tu kutoka hapa madhara yote yanatokea wakati mambo yanayoihusu (mapenzi) hayajakamilika.
7. Usiamini uwongo wa watu wanaochafua maisha, wakisema mapenzi ni uharibifu kwa kusema ukweli, ndani yake kuna urembo, na ndio kwa sababu ina linganishwa na utamu una tokana na mapenzi.
8. Uwe m-angalifu basi, na uone mapenzi kama kitu cha thamana, ambayo lazima itunzwe kwa uangalifu, bila kuifanya iwe kitu cha kutenganisha au kitu cha kuharibu Nguvu.

## XVIII. KUTENDA NA MATENDO YA NGUVU

*Hapo mbele nilikuelezea ya kwamba: “Wakati unapata, nguvu nyingi, furaha na upendo moyo ni mwako au ukisikia uko huru na bila farakano, papo hapo ushukuru kilindini mwako.”*

1. “Kushukurku” ina maanisha kuweka mawazo yako yote kwa mambo ambayo yana pendeza na uyafananishe na maumbo yanayo na maana. Ikiwa hapo awali uliunganisha maumbo na mawazo kwa njia hii, unaweza, ukijikuta kwa mambo magumu, kukanusha hayo mawazo na baada ya hapo yale mambo yanapendeza yaliolekea hapo awali yatainuka. Kwa vile “kuchanuka” kwa mawazo imeongezeka kwa kurudia yaliopita, ina nguvu ya kuondosha mawazo mabaya yanaoletwa na mambo mengine.
2. Kwa hivyo chochote unahitaji kitarudi kutoka ndani yako ikiwa ime ongezeka kwa faida—mradi tu umejiunda ndani yako mambo ambayo yatakusaidia. Haina faida kurudia kusema ya kwamba hili jambo limetumika kitambo (ingawa ilitumika kwa njia isiyo faa) “kuongeza nguvu” maumbo ya nje au watu au kufanya mambo ya ndani kurudi nje, ukiamini yata karibisha maombi na fakara.



## XIX. UFALME WA KILINDI

*Lazima sasa upate kuona vizuri mambo utakabiliana nayo katika ufalme wa kindani ambaye unaweza kujikuta maisha ni mwako mwote na kuimiza kabisa kazi yako. Sina namna ya kueleza ufalme haya isipokua kutumia maumbo, kwa hivi sasa nitatumia viumbe vinaofanana. Haya yanaonekana kwangu yakiwa na vipawa ya “kuiangalia” na kuweka pamoja ufalme na hisia mbali mbali. Njia isiyo halali ya kuunganisha haya ufalme mmoja kwa mwingine sawa sawa ni kama ni nyakati tofauti zikiwa kwa mpangilio moja, inaleta kutoka kwa vitu tulisema hapo awali ambayo tumezoea kutenda tukilinganisha na yale tumezoea kutenda.*

1. Vile nilisema hapo awali, kwa ufalme wa kwanza liitwalo mambo yasio na msimamo, mambo yasio na maana yanatawala. Hapa, kila kitu kiko chini ya utawala wa vitu vya kuguswa, ingawa haya saa zingine haitofautiani na maumbo yasiyo fanana na tamaa hapa, yale unatarajia kufanya na yale umetenda yana kaa katika giza. Kwa hii ufalme kazi yako nikutafakari, ukiwa umepotea katikati ya maumbo ambayo yana badilika. Kutoka hapa unaweza kusonga ukitumia moja ya njia haya mawili: njia ya kifo au njia ya Uzima.
